PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY
Efficient and Fair Appeals Dispensation
PPAA
MAMLAKA YA RUFANI YA ZABUNI ZA UMMA

Toleo Na: 02 Julai - Septemba 2024

# BULLETIN

UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI



*Katibu Mtendaji - PPAA*
*Bw. James Sando*

## Tunaendelea kutekeleza vyema majukumu yetu

**MPENDWA msomaji** karibu katika toleo la pili la Jarida la Mtandaoni kutoka Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA).

Katika jarida hili utapata fursa ya kusoma na kupata uelewa wa majukumu na huduma zinazotolewa na (PPAA) hususan jukumu la kupokea, kusikiliza na kutoa uamuzi wa malalamiko au rufaa zitokanazo na uamuzi wa maafisa masuuli wa taasisi mbalimbali za umma katika michakato ya ununuzi wa umma.

Kupitia Jarida hili utafahamu shughuli zilizofanywa na PPAA kwa kipindi cha miezi mitatu (Julai – Septemba, 2024) katika kuhakikisha Mamlaka inatoa rufaa kwa ufanisi na haki.

Toleo hili ni muendelezo wa toleo lililopita ambapo limelenga kukuhabarisha kuhusu jitahada za PPAA za kuuhabarisha umma juu ya shughuli mbalimbali za Mamlaka ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa habari kwa wadau wa ununuzi na wananchi kwa ujumla.

Karibu tena usome jarida hili ili uifahamu PPAA na shughuli mbalimbali ilizozitekeleza katika kipindi cha miezi mitatu. #Kazilendelee.

# Dkt. Mwigulu aipongeza PPAA kuanzisha Moduli ya kupokea Rufaa Kielektroniki

**WAZIRI wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb.)** ameipongeza Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kwa kuanzisha moduli ya kuwasilisha rufaa/malalamiko kwa njia ya kielektroniki.

Dkt. Mwigulu ametoa pongezi hizo alipotembelea banda la PPAA katika viwanja vya Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC), kabla ya kufunga rasmi Kongamano la 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki, Septemba, 2024.

“Napenda kuwapongeza PPAA kwa kuanzisha moduli hii, nawasihi muendelee kufanya kazi kwa bidii na kuendana na kasi ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,” amesema Dkt. Mwigulu.

Awali, Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando alisema kwa kipindi cha miaka mitatu chini ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, PPAA imefanikiwa kushughulikia jumla ya mashauri 140 yaliyotokana na michakato ya ununuzi wa umma.

“Mheshimiwa Waziri katika mashauri hayo, PPAA ilizuia utoaji tuzo kwa zabuni 32 zenye thamani ya Shilingi bilioni 567 kwa wazabuni wasio na uwezo wa kifedha pamoja na wale waliokosa sifa za kitaalamu za kutekeleza zabuni husika,” amesema Bw. Sando na kuongeza kuwa hatua hiyo imesaidia kuepusha utekelezaji usioridhisha wa miradi unaosababisha upotevu wa fedha za umma na kuchelewesha maendeleo stahiki kwa wananchi.




*Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba (MB.) akimsikiliza Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando katika banda la Mamlaka alipotembelea taasisi hiyo wakati wa Kongamano la 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki lililoanza tarehe 9 -12 Septemba, 2024 katika viwanja vya Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) kabla ya kufunga rasmi Kongamano la 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki lililoanza tarehe 9 -12 Septemba, 2024 jijini Arusha.*

PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY
Efficient and Fair Appeals Disposition
MAMLAKA YA RUFANI YA ZABUNI ZA UMMA
BULLETIN
UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI
PPAA
Toleo Na: 02 Julai - Septemba 2024

# PPAA mguu sawa kutoa elimu kwa wazabuni katika kanda

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA)** imeweka mkakati wa kutoa elimu kwa wazabuni katika kanda zote nchini ikiwa ni jitihada za kuwafikia wadau wa ununuzi wa umma hususan wazabuni.

Akiongea na waandishi wa habari kuhusu mkakati huo, pembeni mwa Kongamano la 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki jijini Arusha, Septemba, mwaka huu, Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando amesema Mamlaka imeweka mkakati huo ili kuzifikia kanda nne (4) ambazo hazijapatiwa elimu ya jinsi ya kuwasilisha mashauri yao pale ambapo hawakuridhishwa na mchakato wa ununuzi.

"Mkakati tulionao kwa mwaka huu wa fedha 2024/25 ni kuhakikisha tunawafikia wazabuni katika kanda nne ambazo hatujazifikia, kwa kufika kwetu katika kanda hizo tutakuwa tumewafikia wazabuni wengi," amesema Bw. Sando.

Bw. Sando ametaja kanda hizo kuwa ni ya Kati, Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini na Kusini.

Wakati huohuo, Naibu Katibu Mtendaji wa PPAA, Bi. Florida Mapunda amezitaja faida za kuanzishwa kwa moduli ya kuwasilisha rufaa/malalamiko kwa njia ya kielektroniki na kueleza kuwa itasaidia kupunguza gharama na muda.

"Moduli hii itasaidia kupunguza gharama na muda kwa kuwa utaratibu wa zamani ulikuwa unamlazimu mzabuni kuwasilisha malalamiko yake katika Ofisi za Mamlaka ya Rufani," amesema Bi. Florida na kuongeza kuwa moduli hiyo itaboresha na kuimarisha uwazi.

Amesema Moduli hii itamwezesha mzabuni au mfanyabiashara kuona hatua kwa hatua jinsi rufaa yake inavyoshughulikiwa hadi utoaji wa hukumu na kuongeza kuwa italeta uwazi na uwajibikaji na hivyo kuwapa imani wazabuni ya kuamini katika mifumo ya utoaji haki kwenye michakato ya zabuni za umma.

Kongamano la Wadau wa Ununuzi wa Umma limewakutanisha wadau zaidi ya 1,500 wa ununuzi wa ndani na nje ya Tanzania. Kaulimbiu ya kongamano hilo ni: "Matumizi ya Dijitali kwa Ununuzi wa Umma Endelevu".



*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) pembeni mwa Kongamano la 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki jijini Arusha, Septemba, 2024.*



*Naibu Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bi. Florida Mapunda akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) pembeni mwa Kongamano la 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki jijini Arusha, Septemba 2024.*


BULLETIN

Dkt. Mwigulu aipongeza PPAA kuanzisha Moduli ya kupokea Rufaa Kielektroniki

BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Florida Mapunda

Mhariri
Gloria Tesha
Mwandishi wa TSN

Wajumbe
Agnes Sayi
Mohamed Makame
Humphrey Kisanga
Violet Limilabo

Katibu
Nelson Kessy

**Mawasiliano:**
Katibu Mtendaji
5 Mkandarasi Place,
Ghorofa ya nne, 58
Barabara ya Lusinde,
S.L.P. 1385, 41104 Dodoma
Simu: +255 (0) 743505505,
Baruapepe: barua@ppaa.go.tz
es@ppaa.go.tz
Tovuti: www.ppaa.go.tz

# PPAA yatoa elimu Kongamano la 16 la Ununuzi wa Umma EAC




**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA)** imeshiriki katika Kongamano la 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki lililowakutanisha wadau wa ununuzi zaidi ya 1,000.

Kongamano hilo limefanyika kwa siku nne jijini Arusha kuanzia Septemba 9 hadi 12 mwaka huu (2024).

Katika kongamano hilo, PPAA imeshiriki kufanya maonesho na kutoa elimu kuhusu majukumu, malengo na mafanikio yake kwa umma na wadau wa sekta ya ununuzi.

Kongamano limewakutanisha wadau wa sekta ya ununuzi wa umma kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Masharik (EAC), ambazo ni mwenyeji Tanzania, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Kenya, Uganda, Rwanda, Somalia na Sudan Kusini.

Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wamepata fursa ya kujadili na kubadilishana uzoefu katika sekta ya ununuzi wa umma katika ukanda huo.

Aidha, taasisi zinazosimamia sekta ya ununuzi wa umma nchini nazo zimepata fursa ya kunadi huduma zake na fursa zinazotolewa.

Taasisi hizo ni PPAA, Mamlaka ya Udhibiti ya Ununuzi wa Umma (PPRA), Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) na Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB).

Kongamano hilo limeongozwa na kaulimbiu isemayo: "Digitalization for Sustainable Public Procurement" (Matumizi ya Dijitali kwa Ununuzi wa Umma Endelevu).

*Washiriki wa Kongamano la 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki lililofanyika jijini Arusha wakipata elimu kuhusu shughuli za PPAA walipotembelea banda la Mamlaka hiyo. Kongamano hilo lilianza tarehe 9 – 12, Septemba 2024.*



# Wadau ununuzi waaswa kutumia moduli kuwasilisha malalamiko kielektroniki

**WADAU wa sekta ya ununuzi** wameaswa kutumia vyema mifumo ya ununuzi kwa njia ya kielektroniki hususan moduli ya kuwasilisha malalamiko na rufaa inayopatikana katika mfumo wa NeST.

Rai hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawalisiliano (Tehama), Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bw. Priscus Kiwango alipokuwa akifunga kikao kazi cha siku nne cha majaribio ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kielektroniki jijini Dodoma, Septemba, 2024.

Bw. Kiwango amesema anaamini kupitia kikao kazi hicho washiriki sasa hawatarudi tena nyuma, bali wataendelea kutumia moduli hiyo kuwasilisha malalamiko na rufaa kwani huokoa muda na gharama.

"Nawiwa kuamini kwamba katika kutekeleza zoezi la kuipitia moduli, mbali na kutoa maoni ya maboresho yanayopaswa kufanyika, mmeweza kujifunza namna moduli hii inavyofanya kazi, hususan kwa kuyaelewa vyema majukumu yenu ninyi kama taasisi nunuzi ambao ni wadau wakubwa katika matumizi ya moduli," alisema Bw. Kiwango.

Pamoja na mambo mengine, amewapongeza wataalamu kutoka Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) na Mamlaka ya Udhibiti ya Ununuzi wa Umma (PPRA) kwa kuandaa moduli hiyo ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa zinazotokana na michakato ya ununuzi wa umma kwa njia ya kielektroniki.

"Hii ni hatua kubwa katika historia ya ununuzi wa umma nchini, hususani katika kuhakikisha kuwa mchakato wa zabuni na malalamiko yanayotokana na michakato hiyo vyote vinafanyika kielektroniki, hongereni sana wataalamu," alisema Bw. Kiwango.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mtendaji wa PPAA, Bi. Florida Mapunda amesema kikao kazi cha upimaji (User Acceptance Test) ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki kilianza tarehe 23 – 26 Septemba 2024 na kimejumuisha washiriki kutoka taasisi 17 za serikali pamoja na wazabuni kutoka kampuni mbalimbali.



*Mkurugenzi wa Tehama, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bw. Priscus Kiwango akitoa hotuba yake kwa washiriki wa kikao kazi cha siku nne cha majaribio ya Moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kielektroniki jijini Dodoma, Septemba, 2024.*



*Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma, Dkt. Frederick Mwakibinga akiongea na wadau wa ununuzi wa umma (hawapo pichani) wakati akifungua kikao kazi cha majaribio ya moduli ya kuwasilisha malalamiko na rufaa kielektroniki jijini Dodoma, Septemba, 2024.*

## PPAA yafanya tathmini ya moduli ya kuwasilisha malalamiko/rufaa kielektroniki

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA)** imeanza kufanya tathmini ya kutumia Moduli ya kupokea na kuwasilisha malalamiko na rufaa kielektroniki katika Mfumo wa Ununuzi wa Umma Kielektroniki (NeST).

Kufanyika kwa tathmini hiyo ni kuashiria muda si mrefu moduli hiyo ya kupokea na kushughulikia malalamiko kielektroniki itaanza rasmi kutumika kama ilivyokuwa imekusudiwa.

Akifungua kikao kazi cha siku nne cha majaribio ya moduli hiyo jijini Dodoma, Septemba, 2024, Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma, Dkt. Frederick Mwakibinga amewasihi wadau wa ununuzi wa umma kukipa uzito kikao kazi cha majaribio ya moduli hiyo ili kuwasaidia katika utendaji wao wa kazi.

"Leo tutakapopitishwa katika moduli hii, tuchukulie kama mafunzo lakini pia tutoe maoni yetu juu ya utendaji wa Moduli hii ili kufikia malengo yaliyotarajiwa na kuiwezesha PPAA kutoa haki kwa wakati na kujenga taswira nzuri ya serikali," amesema Dkt. Mwakibinga.

Naye Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando amesema kikao kazi cha kufanya tathmini ya Moduli hiyo ni matokeo ya ushirikiano kati ya PPAA na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) katika kuhakikisha kigezo cha kupima mfumo kama uko sawa na unaweza kutumiwa na wadau wa ununuzi pamoja na taasisi nunuzi.

"Moduli hii inaokoa muda na kutoa taarifa kwa PPAA kwa wakati kuliko ilivyokuwa awali. Kutokana na mabadiliko ya Tehama ambapo imegusa kila nyanja, hivyo PPAA imejenga moduli hiyo ili kuwawezesha wazabuni wengi zaidi kuwasilisha malalamiko yao kuliko hapo awali," alisema Bw. Sando.

Serikali iliifuta Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 na kutunga Sheria ya Ununuzi wa Umma Na.10 ya Mwaka 2023 ili kukidhi mahitaji ya sasa ambayo yalishindwa kutekelezwa na sheria ya 2011.



*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando akizungumza katika kikao kilichohusisha Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na watumishi wa PPAA katika ofisi za mamlaka hiyo jijini Dodoma, Julai, 2024.*

# PPAA waaswa kuzingatia Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma

**WATUMISHI wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA)** wameaswa kuzingatia kanuni za maadili ya utendaji katika utumishi wa umma wanapokuwa katika majukumu yao kazini.

Rai hiyo imetolewa na Afisa Utumishi kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bi. Mwanadawa Nchembe alipokuwa katika kikao kazi na watumishi wa PPAA jijini Dodoma, Julai, 2024.

Akiongea katika kikao kazi hicho, Bi. Nchembe amesema ni vyema mtumishi unapokuwa kazini kuzingatia kanuni za maadili ya utendaji katika utumishi wa umma kwani kufanya hivyo watumishi na wateja wanapata huduma kwa haki na usawa na pia kunaisaidia serikali kuendeleza azma yake ya utawala bora.

"Azma ya serikali ni kuhakikisha inaimarisha misingi ya utawala bora katika uendeshaji wa shughuli zake kuzingatia kwa sera, sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji na usimamizi wa shughuli za utumishi wa umma na kujenga uwezo wa watumishi wa umma ili watoe huduma bora kwa wananchi, hivyo nawakumbusha kuzingatia miongozo hiyo ili kuendana na maelekezo ya serikali," alisema Bi. Nchembe.

Kwa upande wake Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando amesema watumishi wa Mamlaka hiyo wanazingatia kanuni za maadili ya utendaji katika utumishi wa umma na kwamba wataendelea kuzingatia ili kutimiza azma ya serikali.

"Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kudumisha misingi ya utawala bora ikiwemo haki na usawa, na sisi kama taasisi tutaendelea kufanya kazi kwa bidii na kuhudumia wazabuni na taasisi nunuzi kwa haki na usawa," amesema Bw. Sando.

Kikao hicho cha siku moja kilihudhuriwa pia na Mkurugenzi Msaidizi kutoka Sekretarieti ya Maadili (Utumishi) Bw. Ally Ngonyani, Menejimenti na watumishi wa PPAA.



*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando (Katikati), Afisa Utumishi kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bi. Mwanadawa Nchembe, (kulia) na Mkurugenzi Msaidizi kutoka Sekretarieti ya Maadili (Utumishi) Bw. Ally Ngonyani (kushoto) katika picha ya pamoja na watumishi wa PPAA katika ofisi za mamlaka hiyo jijini Dodoma, Julai, 2024.*

# PPAA kuimarisha ushirikiano na Idara ya Usimamizi wa Sera ya Ununuzi Zanzibar



*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando akizungumza na washiriki wa kikao alipokutana kwa mazungumzo na Kamishna, Idara ya Usimamizi wa Sera ya Ununuzi wa Umma - Afisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar, Bw. Omar Said Omar katika Ofisi za PPAA jijini Dodoma*



*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando (katikati) katika picha ya pamoja na Kamishna, Idara ya Usimamizi wa Sera ya Ununuzi wa Umma - Afisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar, Bw. Omar Said Omar na Naibu Katibu Mtendaji wa PPAA, Bi. Florida Mapunda, Kamishna Msaidizi wa Sera ya Ununuzi wa Umma, Bi. Emma Komba pamoja na watumishi wa PPAA baada ya kuhitimisha kikao kazi katika Ofisi za PPAA jijini Dodoma.*

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA)** imeahidi kuendeleza na kuimarisha ushirikiano na Idara ya Usimamizi wa Sera ya Ununuzi wa Umma katika Afisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar na kuhakikisha kuwa zinaimarisha sekta ya ununuzi.

Ahadi hiyo imetolewa na Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando alipokutana kwa mazungumzo na Kamishna, Idara ya Usimamizi wa Sera ya Ununuzi wa Umma - Afisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar, Bw. Omar Said Omar katika Ofisi za PPAA jijini Dodoma, Julai, 2024.

Bw. Sando amesema kuwa, pamoja na mambo mengine, ziara hiyo imelenga kujifunza na kubadilishana uzoefu katika sekta ya ununuzi wa umma, ambapo Kamishna Omar na ujumbe wake wamejionea jinsi PPAA inavyotekeleza majukumu yake.

"Tumefahamishwa kuwa Zanzibar ina mpango wa kuanzisha chombo kitakachokuwa kinasimamia malalamiko yatokanayo na michakato ya ununuzi wa umma, hivyo sisi kama PPAA tutaendelea kushirikiana nao bega kwa bega kuhakikisha kuwa wanakuwa na chombo madhubuti chenye kusimamia misingi bora ununuzi wa umma," amesema Bw. Sando.

Kwa upande wake Kamishna wa Idara ya Usimamizi wa Sera ya Ununuzi wa Umma - Afisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar, Bw. Omar Said Omar amesema kuwa sekta ya ununuzi Tanzania Bara imeboreshwa vizuri na kupitia ushirikiano baina yake na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) sekta ya ununuzi itaboreshwa zaidi.

"Tunaamini kuwa kupitia ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar utasaidia wananchi na wazabuni kujenga imani na serikali yao lakini pia kuboresha sekta ya ununuzi wa umma kwa ujumla.

Kikao hicho kimehudhuriwa na Naibu Katibu Mtendaji wa PPAA, Bi. Florida Mapunda, Kamishna Msaidizi wa Sera ya Ununuzi wa Umma, Bi Emma Komba, wakuu wa idara na vitengo wa Mamlaka. Kadhalika, ujumbe kutoka SMZ uliongozwa na Kamishna Omar aliyeambatana na maafisa sera watatu ambao ni Asma Ali Mohamed, Wetu Salum Omar na Khamis Makame Ali.

PPAA ni taasisi iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi ya Umma Na. 10 ya Mwaka 2023 ikiwa na jukumu la kupokea na kushughulikia migogoro itokanayo na michakato ya ununuzi wa umma.

# Sheria ilivyochagiza PPAA kuanzisha Moduli ya Rufaa Kielektroniki




*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando akiongea na waandishi wa habari (hawapo pichani) katika banda la PPAA wakati wa Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba, jijini Dar es Salaam, Julai 2024.*

**MABADILIKO ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023** yameisaidia Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kuanzisha Moduli ya kuwasilisha malalamiko na rufaa kielektroniki.

Moduli hiyo inayoleta mapinduzi makubwa kiutendaji kwa PPAA na wadau, inapatikana katika Mfumo wa Ununuzi wa Umma Kielektroniki (NeST).

Mafanikio hayo yamebainishwa na Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando alipotembelea banda la Mamlaka katika Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba jijini Dar es Salaam Julai, 2024.

Bw. Sando amesema mabadiliko ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023, yamesababisha PPAA kuanzisha Moduli ya rufaa zitokanazo na michakato ya zabuni za Umma kielektroniki.

"PPAA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), tumeanzisha Moduli hiyo ambayo inapatikana katika mfumo wa NeST," alisema Bw. Sando.

"Kuanzishwa kwa moduli hiyo kuna faida kadhaa ikiwa ni pamoja na kuokoa muda, gharama na kuongezeka kwa wazabuni," aliongeza Bw. Sando.

Pamoja na mambo mengine, Bw. Sando amesema PPAA ipo katika hatua za mwisho kukamilisha Kanuni za Ununuzi wa Umma za Uwasilishaji wa Rufaa za Zabuni za Umma za Mwaka 2024.




*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando akizungumza na watumishi wa Mamlaka hiyo alipotembelea banda la Mamlaka wakati wa Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba, jijini Dar es Salaam, 2024.*

# PPAA yapongezwa kuanzisha moduli ya kushughulikia rufaa / malalamiko



*Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Omolo akimsikiliza mtumishi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. Stanley Jackson alipotembelea banda la Mamlaka hiyo katika Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba jijini Dar es Salaam, 2024*

**NAIBU Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Omolo** ameipongeza Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kwa kuanzisha Moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki.

Bi. Omolo ametoa pongezi hizo alipotembelea banda la PPAA katika Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba jijini Dar es Salaam, 2024.

Pamoja na mambo mengine, Bi. Omolo amefahamishwa majukumu na mafanikio ya PPAA kwa kipindi cha miaka mitatu chini ya uongozi imara wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

# PPAA yatoa elimu zaidi Sabasaba



*Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo TIB, Bi. Lilian Mbassy akipokea nyaraka zinazoelezea majukumu na malengo ya Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kutoka kwa Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma - PPAA, Bw. Nelson Kessy alipotembelea banda la Mamlaka hiyo katika Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba jijini Dar es Salaam, 2024. Kulia ni mtaalamu wa Ununuzi na Ugavi – PPAA, Bw. Stanley Jackson.*

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA)** imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu, malengo na mafanikio yake kupitia Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba, Dar es Salaam.

Kupitia maonesho hayo ya Sabasaba mwaka huu, viongozi, wananchi, wazabuni, taasisi nunuzi na wadau wa sekta ya ununuzi wa umma waliotembelea banda la Mamlaka hiyo wamepata elimu ya kina kuhusu PPAA na majukumu yake na kuongeza zaidi uelewa wao.

Miongoni mwa viongozi waliotembelea banda la PPAA katika Sabasaba ni Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo TIB, Bi. Lilian Mbassy ambaye amejionea shughuli na majukumu ya Mamlaka hiyo.

Pamoja na mambo mengine, pia Bi. Mbassy amepata fursa ya kuelezewa majukumu na malengo ya PPAA kutoka kwa maafisa wa Mamlaka na kuwapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya.

# CAG atoa kongole kwa PPAA

**MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG),** Bw. Charles Kichere ameipongeza Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu yake.

Bw. Kichere ametoa pongezi hizo wakati alipotembelea banda la PPAA katika Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba jijini Dar es Salaam, mwaka huu.

Pamoja na mambo mengine, Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Huduma ya Sheria PPAA, Bi. Agnes Sayi akizungumza kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando amemueleza CAG kuwa Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 imeboresha masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja kupunguzwa kwa muda wa kushughulikia malalamiko na rufaa zinazotokana na michakato ya ununuzi wa umma kutoka siku 45 hadi siku 40.

"Mabadiliko ya sheria ya ununuzi yamekuwa yakifanyika mara kwa mara kwa lengo la kupunguza muda, kuongeza uwazi na usawa katika shughuli za ununuzi wa umma na kuongeza ushindani," alisema Bi. Sayi.

Kadhalika Bi. Sayi ameongeza kuwa PPAA imefanikiwa kuanzisha Moduli ya kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki ambapo moduli hiyo ipo katika mfumo wa ununuzi wa umma kielektroniki (NeST) ambapo kupitia moduli hiyo wazabuni watawasilisha malalamiko yao kielektroniki jambo ambalo litasaidia kuokoa muda na gharama.




*Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Bw. Charles Kichere akisaini kitabu cha wageni katika banda la Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) katika Maonesho ya 48 Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam maarufu Sabasaba jijini Dar es Salaam mwaka huu.*




*Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Bw. Charles Kichere akimsikiliza Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Huduma ya Sheria wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bi. Agnes Sayi alipotembelea banda la mamlaka katika Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba jijini Dar es Salaam, mwaka huu.*

# Wazabuni wapewa somo moduli ya rufaa kielektroniki




*Watumishi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) wakimpatia maelezo mzabuni aliyetembelea banda la Mamlaka hiyo kwa ajili ya kupata elimu kuhusu moduli mpya ya kuwasilisha rufaa/malalamiko kwa njia ya kielektroniki katika Maonesho ya Kilimo ya Kimataifa ya Nanenane jijini Dodoma, Agosti, 2024.*

**WAZABUNI wameendelea kutembelea Banda la Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA)** na kupatiwa elimu juu ya moduli mpya ya kuwasilisha rufaa/malalamiko kwa njia ya kielektroniki (Complaint & Appeal Management).

Moduli hiyo inarahisisha uwasilishaji wa malalamiko na kutoa fursa kwa wazabuni wengi zaidi kuwasilisha malalamiko yao. Moduli hiyo ni rafiki na inaokoa muda wa kuwasilisha rufaa au malalamiko.

Aidha, moduli hiyo imewekwa kwenye Mfumo wa Ununuzi wa Umma Kielektroniki (NeST) uliojengwa chini ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

PPAA wametoa elimu hiyo katika Maonesho ya Kilimo ya Kimataifa ya Nanenane, katika viwanja vya Nzuguni, jijini Dodoma kuanzia tarehe 01 – 10 Agosti, 2024 katika banda la Mamlaka lilikuwepo katika banda kuu la Wizara ya Fedha.

Kaulimbiu ya Maonesho ya Nanenane 2024 ni "Chagua Viongozi Bora wa Serikali za Mitaa kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi".



*Watumishi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) wakimpatia maelezo Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi kutoka Mamlaka ya Udhibiti ya Ununuzi wa Umma (PPRA), Bw. Robert Kitalala alipotembelea banda la Mamlaka hiyo wakati wa Maonesho ya Nanenane na kupata elimu kuhusu moduli mpya ya kuwasilisha rufaa/malalamiko kwa njia ya kielektroniki katika Maonesho ya Kilimo ya Kimataifa ya Nanenane jijini Dodoma, Agosti, 2024.*

# PPAA yazuia bilioni 261/- michakato ya ununuzi wa umma

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA)** imefanikiwa kuzuia utoaji tuzo kwa zabuni 32 za thamani ya TZS. 261,902,543,425.59 (Sh bilioni 262) kwa wazabuni wasio na uwezo wa kifedha pamoja na waliokosa sifa za kitaalamu za kutekeleza zabuni husika kwa kipindi cha miaka mitatu (2021 – 2024).

Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando amebainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari katika Maonesho ya Kilimo ya Kimataifa ya Nanenane katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma, Agosti, 2024.

"PPAA imeendelea kudhibiti taasisi nunuzi kukiuka taratibu za kisheria hasa katika kufanya tathmini ya zabuni (tender evaluation); katika baadhi ya mashauri ambapo ilifanikiwa kubaini ukiukwaji wa taratibu za kufanya tathimini uliofanywa na taasisi nunuzi ikiwemo kutokuzingatia vigezo vilivyowekwa katika kabrasha la zabuni au kuongeza vigezo vipya ambavyo havikuwepo awali," amesema Bw. Sando.




*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) katika banda la Mamlaka hiyo, Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma, Agosti, 2024 katika Maonesho ya Kilimo ya Kimataifa Nanenane.*

Bw. Sando ameongeza kuwa kwa kufanya hivyo, Mamlaka hiyo ilihakikisha kuwa zabuni zinatolewa kwa wazabuni wenye sifa na hivyo kuiwezesha serikali kupata thamani halisi ya fedha na kuepusha upotevu wa fedha za serikali kiasi cha TZS. 261,902,543,425.59 katika michakato ya ununuzi wa umma kwa kipindi cha miaka mitatu (2021-2024).

"PPAA imeweza kushughulikia jumla ya mashauri 140 yaliyotokana na michakato ya ununuzi wa umma kwa kudhibiti utoaji wa tuzo kwa wazabuni ambao walipendekezwa kupata zabuni bila kuwa na sifa stahiki," ameongeza Bw. Sando.

Aidha, Bw. Sando amesema PPAA ilizuia utoaji tuzo kwa wazabuni 32 wasio na uwezo wa kifedha pamoja na wale waliokosa sifa za kitaalamu za kutekeleza zabuni husika na kuiwezesha serikali kupata thamani halisi ya fedha. Hatua hiyo iliepusha utekelezaji usioridhisha wa miradi ambao ungesababisha upotevu wa fedha za umma na kuchelewesha maendeleo kwa wananchi.

"Serikali ya Awamu ya Sita inaamini kuwa usuluhishi wa migogoro hauwezi kupatikana penye ubaguzi na pale ambapo kuna wanaokosa fursa na haki zao za kiuchumi na kiraia. Hivyo, kitendo cha PPAA kuzuia utoaji wa tuzo kwa wazabuni 32 waliokosa sifa kinaweka uzito katika usuluhishi wa migogoro ambayo ni moja kati ya falsafa za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan," amesema Bw. Sando.

Katibu huyo Mtendaji wa PPAA ameongeza kuwa Mamlaka hiyo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imejenga moduli mpya ya kuwasilisha Rufaa/Malalamiko kwa njia ya kielektroniki (Complaint & Appeal Management).

"Moduli hiyo inarahisisha uwasilishaji wa malalamiko na kutoa fursa kwa wazabuni wengi zaidi kuwasilisha malalamiko yao, ni rafiki na inaokoa muda wa kuwasilisha rufaa," amesema Bw. Sando.

Aidha, moduli hiyo imewekwa kwenye Mfumo wa Ununuzi wa Umma Kielektroniki (NeST), uliojengwa chini ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

PPAA ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Fedha iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi ya Umma Na. 3 ya Mwaka 2001 ambapo baada ya Sheria hiyo kufutwa, Mamlaka ya Rufani ilihuishwa chini ya Sheria ya Ununuzi ya Umma Na. 21 ya Mwaka 2004 na kuhuishwa tena kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 baada ya Sheria Na. 21 ya Mwaka 2004 nayo kufutwa.

Mwaka 2023 Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 nayo ilifutwa na Mamlaka ya Rufani ilihuishwa tena kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 10 ya Mwaka 2023.

# HABARIPICHA



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bw. Elijah Mwandumbya akiwasikiliza watumishi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) alipotembelea banda la Mamlaka hiyo katika Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba, jijini Dar es Salaam, mwaka huu.*



*Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA), Profesa Geraldine Rasheli akisaini kitabu cha wageni alipotembelea banda la Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) katika Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba, jijini Dar es Salaam, Julai mwaka huu.*



*Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Bw. Denis Simba akiwaeleza jambo watumishi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) alipotembelea banda la Mamlaka hiyo katika Maonesho ya Wakulima Nanenane katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma, Agosti mwaka huu.*



*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando katika picha ya pamoja na watumishi wa Mamlaka hiyo jijini Dodoma, Julai, 2024*